

SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 2 Mwaka wa 2



Maswali

1. Watu wa Yeriko walikuwa na shida gani?
2. Elisha aliwasaidia namna gani?
3. Mjane maskini alikuwa na shida gani?
4. Elisha alimsaidia namna gani?
5. Kitoweo chenye walitengenezea manabii kilikuwa na shida gani?
6. Elisha alifanya nini ndio kitoweo kikawa salama?
7. Mtu aliletea Elisha zawadi gani?
8. Watu wangapi walikuwa wanasikiliza Elisha?
9. Elisha aliwalisha namna gani?
10. Elisha alitumia nguvu za Mungu kwa nini?

Majibu

1. Maji ya Yeriko yalikuwa mbaya. Mimea hazikua.
2. Elisha alimwaga chumvi ndani ya chemichemi. Mungu alifanya maji yakawa salama.
3. Mjane alikuwa na deni. Mdeni angechukua wanawe na awauze.
4. Elisha alimwambia cha kufanya. Aliomba vyombo vingi. Mafuta yake kidogo ilijaza vyombo vyote. Aliuza mafuta na akalipa deni.
5. Mtu aliweka vibuyu vya sumu ndani ya kitoweo kwa makosa.
6. Elisha aliomba Mungu. Aliweka unga ndani ya kitoweo na kikawa kizuri.
7. Mtu alileta mikate ishirini ya shayiri na masuke ya ngano.
8. Watu 100 walikuwa wanasikiliza Elisha.
9. Elisha aliomba Mungu. Mungu alifanya mikate ikalisha watu 100.
10. Elisha alitumia nguvu za Mungu kusaidia watu na kuonyesha kwamba Mungu ni Mungu wa kweli.

73 Miujiza ya Elisha

Kwa Biblia

2 Wafalme mlango wa 2:19—22 na mlango wa 4

Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Elisha alitumia nguvu za Mungu kusaidia watu. Aliwaonyesha kwamba Mungu ni Mungu wa kweli

Somo

Elisha alikaa Yeriko na manabii. Watu wa mji walimkujia Elisha. Walisema, "Mji wetu wa Yeriko uko pahali pazuri. Kuna maji mengi. Lakini kuna shida. Maji yanafanya watu kuwa wagonjwa. Maji yanazuia mimea kukuwa."

Elisha aliwambia, "Leta bakuli na chumvi juu yake." Elisha alipeleka hiyo bakuli kwa chemichemi ya maji. Alimwaga hiyo chumvi kwa maji. Akasema, "Mungu ameponya haya maji." Maji yalipona na hayakuwa na ugonjwa tena. Mimea ilikuwa vizuri.

Nabii mmoja alikuwa amekufa. Mjane wake alikuja kwa Elisha. Aliuliza Elisha amsaidia. Huyo mjane alikuwa maskini sana. Alikuwa na deni la mtu. Huyu mtu alikuwa anakuja kuchukua wanawe wawili. Ilikuwa awachukue aende kuwauza kama watumwa kwa sababu ya hilo deni. Mjane alilia Elisha amsaidie.

Elisha aliuliza huyo mjane, "Una nini kwa nyumba yako?" Mjane alimjibu, "Sina kitu chochote ila mafuta kidogo."

Elisha alimwambia aende kwa majirani wake wote. Lazima aombe vyombo vingi sana vyenye havina maji. Elisha alimwambia aende ndani ya nyumba yake na afunge mlango. Halafu amwage mafuta kwa kila chombo.

Mjane alifanya vile Elisha alimwaagiza. Aliomba vyombo vingi vilivyokuwa tupu kutoka kwa majirani wake. Mjane aliingia ndani ya nyumba pamoja na wanawe na wakafunga mlango. Mjane alimwaga mafuta kwa vyombo tupu. Wanawe walimsaidia. Kila chombo kilipojaa mafuta, waliiweka kando.

Wanawe waliendelea kumletea vyombo. Mjane aliendelea kumwaga mafuta. Vyombo vyote vilipojaa, mjane aliambia mwanawe, "Leta chombo kingine." Alimjibu, "Hakuna chombo kilicho tupu. Vyombo vyote vimejaa." Halafu mafuta yakakoma. Mungu alikuwa amefanya chombo kimoja kidogo cha yule mjane, kujaza mafuta kwa vyombo vingine vyote!

Mjane alirudi kwa Elisha. Alimwambia kwamba vyombo vyote vimejaa mafuta. Elisha aliambia yule mjane aende auze hayo mafuta. Mjane alienda akaiza mafuta. Halafu alipata pesa nyingi ya kulipa deni lake. Alibaki na pesa zingine za matumizi yake pamoja na wanawe.

Elisha alizuru Gilgali kuona manabii. Kulikuwa na njaa kwa hiyo nchi. Watu walikuwa na njaa. Elisha aliambia watumishi wake watengenezee manabii kitoweo kwa sufuria kubwa.



Nabii mmoja alienda kondeni kutafuta chakula ili aweke ndani ya hicho sufuria. Alipata mzabibu mwitu. Alichuna vibuyu vya huo mzabibu. Alizichukua na akaenda kuweka kwa hicho kitoweo. Hakujua kwamba zilikuwa sumu.

Kitoweo kilimiminwa. Manabii walianza kukula kitoweo. Mmoja wao alipaza sauti, "Kuna sumu kwa kitoweo." Manabii hawangeweza kula kitoweo. Walikuwa na njaa sana.

Elisha aliwambia kuleta unga kidogo. Aliomba Mungu. Aliweka unga ndani ya hicho kitoweo. Akasema, "Mimina hicho kitoweo." Kitoweo kilikuwa kizuri. Kilikuwa sawa cha kukula.

Kuna mtu aliyeletea Elisha zawadi. Alimletea mikate ishirini ya shayiri na masuke ya ngano. Elisha alikuwa anafundisha watu. Watu karibu mia moja walikuwa wakimsikiliza. Hao watu wote walikuwa na njaa.

Elisha aliambia mtumishi wake kugawa hicho chakula cha zawadi. Elisha alimwambia apee kila mtu chakula akule. Lakini mtumishi wake alisema, "Ninaweza kugawa watu mia moja chakula namna gani? Mikate midogo ishirini haiwezi kulisha watu wengi."

Elisha alimwambia, "Wape watu wote chakula wale. Hivyo ndivyo Mungu anasema. 'Wote watakula cha kutosha na kingine kitabaki.'" Watumishi walipeana hiyo mikate ishirini ya shayiri na masuke ya ngano. Mungu alitengeneza chakula cha kutosha watu mia moja kula. Kulikuwa na kilichobaki.

Elisha alitumia nguvu za Mungu kusaidia watu wengine na kuwaonyesha kwamba Mungu ni Mungu wa kweli.